HALI HALISI YA RASLIMALI ZA MIFUGO NCHINI

na

Pius Lazaro Mwambene

TALIRI Uyole

1. UTANGULIZI

Tanzania ina raslimali nyigi za mifugo, kama ifuatavyo:

- Ng'ombe: ~25.8m (> 95% ni ng'ombe wa asili)
- Mbuzi na kondoo: 18.8m (88% ni mbuzi)
- Kuku wa asili: karibu 40m
- Nguruwe: karibu millioni 2.4*, na
- Koosafu zingine tofauti za mifugo

Idadi ya Mifugo katika Kanda (2012)

Aidha, idadi ya mifugo katika Kanda yetu ni kama ifuatavyo:

- Ng'ombe ni 2.2m (17% ya idadi ya nchi)
- Karibu 95% ya idadi hii ni wale wa asili, 4.7% ni wa maziwa (hasa chotara) na 0.3% ni wa nyama
- Mbuzi na kondoo ni karibu 1.8m (11% ya idadi yote)
- Kuku ni karibu 9.2m (karibu 15.3% ya idadi ya nchi)
- Nguruwe ni karibu 0.9m (karibu 65% ya idadi yote)

- Mifugo mingi ya asili imeendelezwa katika mazingira ya kitropic na hivyo kuweza kuhimili.

- Hata hivyo uzalishaji wao ni mdogo ukilinganisha na mifugo iliyoendelezwa katika nchi zilizoendelea.

- Mifugo mingi (≈ 94%) bado inafugwa katika mifumo ya ufugaji wa asili.

- Hivyo juhudi zinahitajika ili kuboresha uzalishaji na hatimaye kuchangia kwenye pato la mfugaji na taifa.

- Mambo makuu ya kuzangatia: **lishe/matunzo, mbegu bora, afya, usindikaji na masoko**

Mchango wa Sekta ya Mifugo kwenye Pato la Taifa ni mdogo sana (2016):

- 16% kwenye pato la sekta ya kilimo
- 7.4% kwenye pato la Taifa,
- Inachangia maisha ya takribani 50% ya kaya za wakulima (kaya 62% vijijini na kaya 23% mjini).
- Inachangia pia kwenye usalama wa chakula, kipato, kilimo, jamii, kama benki, tahadhali, nishati, n.k.

- Sekta inakua kwa 2.2% kwa mwaka, hasa kutokana na ongezeko la idadi ya mifugo kuliko uzalishaji/tija kwa mnyama.

- Ulaji wa mazao ya mifugo bado ni mdogo nchini. Mwaka 2016 ulaji ulikuwa lita **47** za maziwa, kilo **12** za nyama na mayai **75**.

- Viwango vinavyoshauriwa na FAO ni lita 200 za maziwa, kilo 50 za nyama na mayai 300 kwa ajili ya afya na ukuaji bora.

Sababu za sekta kukua kidogo na kutoa mchango mdogo

- Uwekezaji mdogo kwenye sekta na hivyo kusababisha viwango duni vya uzalishaji, mfano;

- Uzalianaji mdogo wa mifugo kwa mwaka (40 – 50%),
- Vifo vingi vya mifugo (30 - 40%),
- Uvunaji mdogo wa mifugo (< 10% kwa ng'ombe)
- Muda mrefu zaidi kati ya mizao (> miezi 18 kwa ng'ombe)
- Muda mrefu kufikia uzito wa kuvunwa (> miaka 6)
- Uzito mdogo wakati wa kuvuna
- Mazao kidogo na hafifu ya mifugo, yasiokuwa na soko zuri hasa la nje

Hivyo ili sekta iweze kukua juhudi za makusudi zinahitajika ili kuboresha viwango hivi vya uzalishaji

2. MAKUNDI YA NG'OMBE WANAOFUGWA NCHINI

- **Kundi la kwanza:** Ng'ombe wa asili aina ya zebu (wana nungu kubwa na pembe fupi): Iringa (wekundu), Chaga, Pare, Gogo, Mbulu, Singida (weupe), Mkalama, Maasai na Zanzibar.

- Ng'ombe hawa ndio wengi (>95%) na wametawanyika karibu nchi nzima

- Wanastahimili mazingira ya kitropic vizuri ikiwa ni pamoja na magonjwa, lishe duni, joto, ukame n.k.

- Wanafugwa hasa kwa ajili ya nyama, maziwa na shughuli za kilimo na kijamii

- **Kundi la Pili:** Ng'ombe aina ya sanga (Ankole)
  - Ng'ombe hawa wanapatikana zaidi Kagera, Kigoma, Tabora, Geita, Katavi na Rukwa.
  - Wana nundu ndogo, pembe kubwa na ndefu.
  - Wanafugwa hasa kwa ajili ya nyama na maziwa

- **Kundi la tatu:** Ng'ombe aina ya zenga (Fipa, Tarime na Sukuma)
  - Wana mchanganyiko wa damu ya sanga na zebu.
  - Wana nundu ndogo, pembe saizi ya kati na ndefu

- **Ng'ombe wa kifipa anafugwa zaidi katika mikoa ya Rukwa, Songwe na Katavi.**

- Ng'ombe huyu ametafitiwa zaidi na taarifa zake za kimaumbile na kivinasaba tunazo

- Kutokana na sifa yake ya uzalishaji wa maziwa zaidi, sasa tunamtumia kuzalisha madume na majike chotara kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa maziwa nchini

- Ng’ombe aina ya Tarime wako zaidi mkoani Mara, ingawa kwa sasa wametawanyika hadi Kusini Magharibi na pia kusini mwa nchi

- Ng’ombe wa Kisukuma wako zaidi Kanda za ziwa ingawa nao wametawanyika hadi Kusini Magharibi na kusini mwa nchi

❑ **Kundi la nne:** Ng’ombe aina ya Mpwapwa

➢ Ni ng’ombe aliyezalishwa kutokana na kuchanganya damu ya Zebu, Sahiwal, Red Sindi, Ayrshire na Boran.

➢ Amezalishwa kwa ajili ya nyama na maziwa hasa, katika nyanda kame (Dodoma na Singida)

- **Kundi la tano:** ng’ombe wa maziwa kutoka nje, hasa aina ya Friesian, Ayrshire, Jersey, Guernsey na Sahiwal.

- **Kundi la sita:** Ng’ombe wa nyama kutoka nje, hasa aina ya Boran, Simmental na Angus.

- Hawa ni ng’ombe walioletwa nchini kwa ajili ya aidha kuongeza uzalishaji wa maziwa au nyama.

- Ng’ombe wa maziwa na chotara wao wanafugwa zaidi na wafugaji wadogo wadogo, LMUs, mashamba binafsi

- Ng’ombe wa nyama wanafugwa zaidi na mashamba ya serikali hasa kwenye ranchi za Taifa.

4. BAADHI YA NG'OMBE WALIOPO NCHINI

Ufipa:

- **Rangi mbalimbali (hasa nyekundu na mchanganyiko wa nyeusi na nyeupe, nyeusi na mchanganyiko wa nyekundu na nyeupe).**
- **Ukubwa: saizi ya kati**

Iringa wekundu:

- Kutoka mikoa ya Iringa na Njombe
- Rangi moja nyekundu au nyekundu na nyeusi
- Ukubwa: saizi ya kati

Singida (weupe)

- Kutoka mkoa wa Singida
- Rangi nyeupe na ukijivu kidogo maeneo ya shingo
- Ukubwa ni saizi ya kati

Ugogo

- Kutoka Dodoma na sehemu za mikoa ya Iringa na Morogoro
- Rangi mchanganyiko (hasa nyeusi, kahawia, kijivu au mchanganyiko)
- Ukubwa: saizi ndogo

Ankole

- Rangi: Nyekundu
- Ukubwa: saizi ya kati

Zanzibar

- Rangi mbalimbali na hasa nyeusi na mabaka meusi na meupe
- Ukubwa: saizi ya kati

Mpwapwa:

- Rangi mbalimbali (hasa nyekundu na kahawia)
- Ukubwa: saizi ya kati

Boran

- Rangi mbalimbali (hasa nyeupe, kijivu au kahawia)
- Ukubwa: saizi Kubwa

5. Wastani wa Uzito na Ukuaji wa ng'ombe wa asili

UKOO	UZITO (KUZALIWA)		UZITO (>MIAKA 4)		UKUAJI/ SIKU	
	JIKE	DUME	JIKE	DUME		MAZIWA
FIPA	18	20	280	360	360g	4
ANKOLE	20	22	320	400	4OOg	2
TARIME	16	18	250	300	320g	1.5
SUKUMA	18	20	270	350	330g	3
MPWAPWA	22	24	350	400	500g	6
SINGIDA	17	19	260	320	320g	2
UGOGO	15	17	230	280	300g	1.5
IRINGA	18	20	270	330	320g	2
MAASAI	18	21	320	380	370g	2
BORAN	23	25	400	> 600	> 700g	3
MBULU/CHAGA/PAR	-	-	-	-	-	-

Zebu/Sanga/Zenga: Wanastahimili sana mazingira ya kitropic, magonjwa na visumbufu. Hivyo udhibiti wa magonjwa hasa ya kupe na ndorobo ni nadra isipokuwa hutibiwa wakiugua. Wengi wana kinga ya asili hasa ya magonjwa ya kupe na ndorobo

Mpwapwa/Boran: Wanahitaji uogeshaji wa mara kwa mara ili kudhibiti magonjwa hayo

6. Dalili za kutoweka kwa baadhi ya Mifugo yetu nchini – Mwaka 2010

Ukoo	Idadi (Jike Wazazi)	Maoni
Chaga/Par/Mkalama/Mpwapwa	**< 1000 kwa kundi**	**Wako katika Hatari Zaidi ya kupotea**
Mbulu/Ugogo/ Singida Weupe	**< 10,000 kwa kundi**	**Wanahitaji kuchukua tahadhari mapema**
Fipa	**> 100,000**	Bado wako salama kiasi. Lakini tishio lao kubwa ni mwingiliano kati ya makundi haya na hata ya nje na hivyo kuanza kupoteza uhalisia wa kila kundi. Pia wafugaji wetu kuendelea kufuga kienyeji sana kwa sababu ya kukosa elimu
Ankole	**> 100,000**	
Iringa Wekundu	**> 100,000**	
Tarime	**> 100,000**	
Sukuma	**> 100,000**	
Boran	**> 100,000**	
Maasai	**> 100,000**	

7. SABABU ZINAZOASHIRIA KUTOWEKA KWA MIFUGO YETU:

- Mwingiliano, upandishaji holela, na elimu duni ya uendelezaji wa kizazi/koo
- Makundi mengi kutokuwa na mipango ya kuiendeleza kwa ajili ya matumizi ya sasa na baadaye (elimu, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini)
- Uingizaji holela wa koo zingine, hasa za nje (bila sera/ utaratibu/usimamizi makini)
- Kupungua kwa maeneo ya malisho kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kilimo, idadi ya watu na hifadhi za wanyamapori/misitu.

Hivyo ni budi kuitunza mifugo yetu hasa ya asili ili:

- Kuendelea kuhimili:
– mabadiliko ya tabia-nchi na mifumo ya uzalishaji
– mabadiliko ya mahitaji ya soko

- Kuwa na wigo mpana wa kuchagua aina tofauti za mifugo kwa ajili ya matumizi ya sasa na ya baadaye

- Kulinda sifa zao za msingi hasa zinazopendwa na wafugaji wenyewe pamoja na soko

- Kulinda umuhimu wa matumizi yao hasa ya kijamii, kiuchumi, kiutamaduni, kimazingira na kihistoria

- Kulinda utajiri wa wafugaji wenyewe na nchi kwa ujumla

Mbinu tofauti za uboreshaji wa koosafu zetu

- Kufanya uchambuzi ndani ya makundi yenyewe (nyama, maziwa au vyote)
- Kuzalisha ng'ombe chotara kati ya majike ya asili na mbegu za kisasa (aidha nyama au maziwa)
- Kutumia ng'ombe walioboreshwa tayari (Mpwapwa, Boran, Sahiwal, Gir, Friesian, Ayrshire, Jersey, Guernsey etc.)

Kwa mazingira ya mkoa wa Rukwa:

- Ng'ombe bora wa maziwa ni chotara kati ya asilimia 40 – 70% ya damu ya kisasa
- Maziwa na nyama (dual): Mpwapwa, Sahiwal, Gir
- Nyama: Boran, Fipa, Ankole, au chotara wao na wale wa nyama

AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA